SEBHA UNIVERSITY JOURNAL OF HUMAN SCIENCES VOL.24 NO. 2 2025
DOI: 10.51984/JOHS.V24I2.3582

مجلة جامعة سبها للعلوم الإنسانية
Sebha University Journal of Human Sciences

Journal homepage: [http://www.sebhau.edu.ly/journal/johs](http://www.sebhau.edu.ly/journal/johs)



# KUCHUNGUZA UJENZI WA DHAMIRA ZA METHALI KATIKA DIWANI YA SAADANI KANDORO KATIKA MUKTADHA WA JAMII YA KISASA

Ahmed Emhemad Badda

Department of Languages and African Studies, Faculty of Languages, University of Sebha, Libya

**Maneno Muhimu**
Diwani
Methali
Dhamira
Jamii ya kisasa
Dhamira
Muktadha wa jamii ya kisasa

**MUHTASARI**

Wimbi la sayansi na teknolojia limezikumba jamii nyingi, ikiwepo jamii ya Waswahili. Wimbi hili limezifanya jamii kueleza fikra na mitazamo yao kwa njia ya kijigitali jambo ambalo linachochea mabadiliko ya matumizi ya lugha. Katika muktadha huu methali kama sehemu ya hazina ya fasihi simulizi zinakabiliwa na hatari ya kusahauliwa na kupuuzwa, hasa, na kizazi kipya ambacho ndicho kilichokumbatia zaidi usasa katika mawasiliano na burudani. Pamoja na changamoto hizo, methali bado zinaendelea kuwa ni ghala muhimu lenye kuhifadhi ukweli wa maisha, elimu, maadili na utamaduni wa kijamii. Hivyo basi kazi hii inachunguza ujenzi wa dhamira za methali katika diwani ya Saadani Kandoro katika muktadha wa jamii ya kisasa. Methali, kama sehemu ya urithi wa fasihi na utamaduni wa Kiswahili, zimekuwa na nafasi muhimu katika kuendeleza maadili, mitazamo ya kijamii, na mshikamano wa jamii kwa miongo mingi. Hata hivyo, katika zama za sasa zinazokumbwa na mabadiliko ya kijamii, kiteknolojia na kiutamaduni, matumizi na tafsiri ya methali yanahitaji kuchunguzwa kwa mtazamo mpya. Utafiti huu ulitumia mbinu ya uchanganuzi wa kijamii wa fasihi (sociological literary analysis) kuchambua methali zilizotumika katika mashairi ya Kandoro. Methali 19 ziliteuliwa na kuchambuliwa kwa kuzingatia mchango wake katika kujenga dhamira zinazohusiana na maisha ya jamii ya sasa. Nadharia ya kijamii ya fasihi ilitumika kufafanua namna methali hizi zinavyowasilisha mitazamo ya kijamii, mabadiliko ya maadili, haki, usawa wa kijinsia, na mshikamano wa kijamii. Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa methali katika diwani ya Kandoro bado zina nafasi muhimu katika jamii ya sasa. Methali hizi hutumika kuhamasisha maadili bora, mshikamano wa kijamii, heshima ya binadamu, na haki za kijamii. Aidha, zimejipenyeza katika mawasiliano ya kisasa kupitia majukwaa ya mitandao ya kijamii, memes, na mijadala ya mtandaoni, hivyo kuendelea kuathiri fikra na mitazamo ya kizazi kipya. Kwa ujumla, utafiti huu umebainisha kuwa methali si tu urithi wa kale bali ni zana hai ya kufundisha, kuonya na kuhamasisha jamii katika zama za sasa. Utafiti unapendekeza kuendelezwa kwa matumizi ya methali katika elimu, fasihi, na mawasiliano ya kijamii ili kusaidia kukuza jamii yenye maadili, mshikamano, na heshima kwa utu wa binadamu.

# دراسة معاني الأمثال في الديوان الشعري للروائي سعدان كاندورو

أحمد امحمد امبارك بده

قسم اللغات والدراسات الإفريقية، كلية اللغات، جامعة سبها، ليبيا

**الكلمات الافتتاحية**
مجتمع
ديوان
فكرة
شعر
أمثال

**الملخص**

هدف هذا البحث إلى تحليل كيفية توظيف الأمثال السواحيلية في ديوان سعداني كندورو كأداة للتعبير عن الواقع الاجتماعي والثقافي. ترتكز مشكلة البحث على السؤال: كيف تُستخدم الأمثال في الشعر لنقل رسائل نقدية تتعلق بالمجتمع؟ اعتمد البحث على منهج التحليل السوسيولوجي للأدب، حيث تم اختيار 19 مثلاً من النصوص الشعرية بناءً على تكرارها ودلالتها الاجتماعية. أظهرت النتائج أن الأمثال تُستخدم لتقوية الخطاب الأخلاقي، وتأكيد الهوية الثقافية، وكشف التناقضات في البنى الاجتماعية. توضح هذه النتائج أن الشعر السواحيلي الحديث لا يكتفي بالزينة البلاغية، بل ينخرط في مساءلة الواقع الاجتماعي عبر أدوات تراثية كالْمَثَل.

## Utangulizi

*Corresponding author:
E-mail addresses: [Ahme.baddah@sebhau.edu.ly](mailto:Ahme.baddah@sebhau.edu.ly)
*Article History: Received 05 January 2025 - Received in revised form 08 July 2025 - Accepted 10 July 2025*

Methali za Kiswahili ni sehemu muhimu ya urithi wa fasihi ya Waswahili. Methali hizo, hutumika kueleza maarifa hekima, maadili, na mtazamo wa jamii kuhusu maisha. Aidha, toka azali methali zimekuwa msingi wa mawasiliano ya kijamii na zana ya malezi ya kijamii katika muktadha wa kila siku. Katika fasihi ya Kiswahili, methali hazionekani tu kama maneno ya busara, bali pia kama mbinu ya kisanaa ya kuimarisha uhalisia na ujumbe wa maandishi ya kifasihi. Katika fasihi ya Kiswahili, methali hazionekani tu kama maneno ya busara, bali pia kama mbinu ya kisanaa ya kuimarisha uhalisia na ujumbe wa maandishi ya kifasihi.

Katika karne hii ya ishirini na moja, mabadiliko makubwa ya kijamii na kiteknolojia yameathiri namna methali zinavyotumika na kueleweka. Katika jamii ya kisasa inayotawaliwa na mitandao ya kijamii, utandawazi, na mabadiliko ya mitazamo ya vijana, methali zimepata nafasi mpya kama zana za kuendeleza mawasiliano ya kijamii na mijadala ya kijamii. Kulinga na muktadha husika wakati mwingine zinachapishwa kama memes kwenye mitandao ya kijamii, au semi zinazovuma kwenye majukwaa ya kidijitali. Katika miaka ya hivi karibuni, baadhi ya washairi wa Kiswahili wa kisasa wameanza kutumia methali kama nyenzo ya kuunganisha historia na hali ya sasa ya jamii. Saadani Kandoro ni miongoni mwa washairi wanaotumia mbinu hii kwa ustadi mkubwa. Kazi yake inaonesha namna methali zinaweza kutumika kama daraja kati ya jadi na sasa, zikitoa sauti kwa masuala ya kijamii kama ukosefu wa haki, maadili, na mabadiliko ya kiutamaduni. Methali kwa hivyo hazibaki tu kama kumbukumbu za fasihi ya kale, bali zinabeba hekima hai inayoweza kusaidia kizazi cha sasa. Katika dunia ya sasa inayobadilika kwa kasi, methali hutoa dira ya maadili, mshikamano, na busara ya kijamii. Hivyo basi, kuna haja kubwa ya kuendeleza matumizi ya methali si tu katika sanaa na elimu, bali pia katika mawasiliano ya kila siku ili kuhifadhi urithi wa kitamaduni na kuendeleza mijadala ya kijamii. Kwa mfano, methali kama "Subira huvuta heri" au "Bandu bandu humaliza gogo" bado zina maana pana katika kuhimiza uvumilivu na juhudi endelevu, mambo ambayo ni msingi wa maendeleo binafsi na ya jamii.

Kwa kuzingatia haya, ni wazi kuwa methali zina nafasi muhimu si tu katika uhifadhi wa utamaduni wa Kiswahili, bali pia katika kutoa mwongozo wa kijamii na kimaadili katika nyanja mbalimbali za maisha ya sasa. Hivyo basi, kuna haja kubwa ya kuendeleza matumizi ya methali katika elimu, sanaa, na mawasiliano ya kila siku ili kizazi kipya kipate busara zilizojengwa katika misingi ya jamii zao.

Licha ya tafiti nyingi kuhusu methali, utafiti huu unatofautiana kwa kuangazia matumizi ya methali ndani ya ushairi wa maandishi, jambo ambalo halijapewa uzito wa kutosha katika tafiti zilizotangulia. Hivyo basi, utafiti huu unakusudia kuangalia jinsi nguvu za ujumbe wa methali zinavyotumika kuwasilisha ujumbe unaohusu masuala ya kijamii na kiutamaduni katika ushairi wa Saadani Kandoro.

Kwa kutumia nadharia ya Uchanganuzi wa Kijamii wa fasihi, utafiti huu ulichambua methali zilizoteuliwa ili kufichua uhusiano kati ya lugha ya kishairi na mitazamo ya jamii. Lengo ni kuonesha kuwa methali si kauli zilizopitwa na wakati, bali ni zana hai za kuendeleza mjadala kuhusu maisha ya jamii ya leo.

**Mapitio ya Fasihi**

Tafiti nyingi zilizotangulia zimechunguza matumizi ya methali katika fasihi ya Kiswahili, hususan katika muktadha wa simulizi za jadi. Kwa mfano, Mulokozi (1999) na Khamis (2005) walielekeza tafiti zao kwenye nafasi ya methali katika kueneza hekima ya kijamii, kuimarisha malezi ya kijamii, na kuhifadhi urithi wa kitamaduni miongoni mwa jamii za Waswahili. Vilevile, walichambua mchango wa methali katika mawasiliano ya kila siku, hususan katika kujenga na kudumisha mahusiano ya kijamii.

Hata hivyo, tafiti hizi nyingi zimejikita katika fasihi simulizi na hazijalenga kwa kina matumizi ya methali ndani ya fasihi andishi ya Kiswahili, hasa katika ushairi wa kisasa unaoibua masuala ya kijamii na kisiasa. Utafiti huu unatofautiana na zile zilizotangulia kwa kuwa unachunguza kwa undani jinsi methali zinavyojengwa na kutumika ndani ya *Diwani ya Saadani Kandoro*, ambapo methali hazitumiki tu kama mapambo ya lugha, bali kama mbinu mahsusi ya kifani na kimaudhui katika kufikisha ujumbe unaohusiana na hali halisi ya jamii ya kisasa.

Zaidi ya hayo, utafiti huu unajiegemeza kwenye nadharia ya kijamii ili kuchanganua maana fiche na athari za kitamaduni zilizomo katika matumizi ya methali. Kwa njia hii, utafiti huu unapanua uelewa wetu kuhusu mwingiliano kati ya urithi wa jadi (methali) na maudhui yanayobeba changamoto, matumaini, na migongano ya jamii ya sasa kupitia ushairi wa Kiswahili ulioandikwa.

Kwa hivyo basi, utafiti huu si tu kwamba unaangazia upekee wa matumizi ya methali katika kazi za Saadani Kandoro, bali pia unaweka msingi mpya wa kitaaluma kwa ajili ya tafiti zijazo kuhusu nafasi ya methali katika fasihi andishi ya Kiswahili. Uchanganuzi huu unaonesha namna methali zinavyoendelea kuwa chombo hai cha kuakisi dhamira za kijamii, kiutamaduni, na hata kisiasa katika muktadha wa kisasa.

**Tatizo la Utafiti**

Pamoja na kuwepo kwa tafiti mbalimbali kuhusu methali katika muktadha wa simulizi na mawasiliano ya kijamii, kuna uhaba wa tafiti zinazochunguza kwa kina jinsi methali zinavyojengwa na kutumika ndani ya fasihi ya maandishi ya Kiswahili, hasa ushairi wa kisasa. Katika zama hizi za mabadiliko ya kijamii na kiteknolojia, kuna haja ya kuchunguza jinsi methali zinavyopata maana mpya, namna zinavyochangia ujenzi wa dhamira mbalimbali, na nafasi yake katika mjadala wa kijamii wa sasa.

Utafiti huu unatamani kujibu maswali kama: Je, methali hizi zinabeba dhamira zipi zinazohusu maisha ya sasa? Je, methali zinatumika vipi kuibua mijadala ya kijamii katika zama za mitandao ya kijamii na utandawazi? Na ni kwa namna gani methali zinahifadhi maana ya kihistoria huku zikihudumia mahitaji ya kijamii ya kizazi cha sasa?

Kwa msingi huo, utafiti huu una lengo la kuchunguza kwa kina ujenzi wa dhamira za methali katika diwani ya Saadani Kandoro, ili kubaini namna methali hizi zinavyotumika kama mbinu ya fasihi ya maandishi katika kushughulikia masuala ya kijamii na kiutamaduni katika jamii ya sasa.

**Swali la Utafiti**

Dhamira zipi zinazojengwa kutokana na matumizi ya methali katika diwani ya mashairi ya Saadani Kandoro katika zama hizi za mabadiliko ya kijamii na kiteknolojia?

**Mbinu na Nadharia Zilizotumika**

Utafiti huu umetumia mbinu ya uchanganuzi wa kijamii wa fasihi (sociological literary analysis) ili kuchambua matumizi ya methali katika diwani ya Saadani Kandoro. Njia hii inazingatia jinsi kazi za kifasihi zinavyoakisi hali halisi ya jamii, kwa kuangalia uhusiano kati ya maandishi na mazingira ya kijamii na kitamaduni ambamo kazi hiyo ilitokea. Muktadha wa jamii ya kisasa, yenye mabadiliko ya kijamii na teknolojia ya mawasiliano, ni kiini muhimu katika uchambuzi huu.

Methali 19 zilichaguliwa kutoka katika mashairi ya Kandoro kwa kutumia vigezo vya uhusiano wake na maudhui ya kijamii. Methali zilizoteuliwa ni zile ambazo zinaendelea kuwa na maana na umuhimu katika jamii ya sasa, zikihusiana na masuala kama maadili, haki, mshikamano wa kijamii, jinsia, na mitazamo ya kijamii inayobadilika. Methali hizi pia huchukuliwa kama semi zinazoweza kusambazwa na kutumika katika muktadha wa mawasiliano ya leo kama vile mitandao ya kijamii.

Katika uchambuzi wa data, kila methali ilichunguzwa kwa kuzingatia muktadha wake wa kisanaa, maana yake ya kijamii, na mchango wake katika ujenzi wa dhamira katika mashairi. Uangalifu maalum uliwekwa katika kuchunguza jinsi methali hizi zinavyohusiana na changamoto za kijamii za sasa, kama vile mabadiliko ya maadili, matumizi ya teknolojia, na mitazamo mipya ya kijinsia na kijamii.

Nadharia ya kijamii ya fasihi ilitumika kuelewa jinsi methali hizi zinavyotumika kama zana za ukosoaji wa kijamii na ujenzi wa utambulisho wa jamii ya Waswahili katika zama za sasa. Utafiti huu unatambua kuwa kazi ya fasihi ni kioo cha jamii na kwamba methali zinazotumika leo huibua mijadala muhimu kuhusu maisha ya kisasa katika zama hizi tulilizo nazo za kidijitali.

Methali zimechambuliwa kama mihimili muhimu ya ujenzi wa dhamira zinazojitokeza katika *Diwani ya Saadani Kandoro*, hutumika kuakisi changamoto na mivutano ya jamii ya sasa. Kwa mfano, methali "Mti wenye matunda hupigwa mawe" imetumika kufichua dhamira ya wivu, chuki na unyanyasaji dhidi ya watu wenye mafanikio katika jamii ya kisasa, ambapo mafanikio binafsi mara nyingi huibua visasi na husuda badala ya kupongezwa.Ama methali "Samaki mkunje angali mbichi" imeangaziwa kama msingi wa dhamira ya malezi bora**,** inayosisitiza umuhimu wa ukuzaji wa watoto wenmye misingi ya maadili wakiwa wadogo, ili wanapoendele kukua wawe raia wema katika jamii inayoendelea kukumbwa na mmomonyoko wa maadili kutokana na athari za utandawazi na mitandao ya kijamii.

Uchanganuzi huu umeonesha kuwa methali zinazotumika na mshairi hazipo kama mapambo ya lugha pekee, bali ni zana mahsusi za kimfumo za kuwasilisha ujumbe wa kijamii**,** ukosoaji wa mienendo isiyofaa, na kuimarisha utambulisho wa jamii ya Kiswahili. Kwa kutumia methali, mshairi anajenga dhamira zinazohusiana moja kwa moja na mazingira halisi ya kijamii na kihistoria ya msomaji wa leo, hivyo kuzifanya kuwa nyenzo hai za mawasiliano na ujenzi wa jamii katika muktadha wa kisasa.

**Dhamira katika Methali**

Katika sehemu hii tumewasilisha, kuchambua na kujadili data za utafiti zinazohusiana na dhamira zinazojengwa kupitia methali katika diwani ya Mashairi ya Saadani. Dhamira huelezwa kuwa ni wazo, mawazo au lengo na nia ya mtunzi au msimulizi wa kazi ya fasihi pale anapotunga kazi yake na kutaka lengo hilo liwafikie na kutambuliwa na hadhira yake (Njogu na Chimerah, 1999). Katika hali ya kawaida dhamira huusisha dhamira kuu na ndogondogo ambazo kwa ujumla wake ndio hujenga sehemu ya maudhui ya kazi husika ya fasihi. Methali zilizotumika katika diwani ya Mashairi ya Saadani zimetoa mchango mkubwa katika kujenga na kuibua dhamira mbalimbali kwa wasomaji wa mashairi hayo. Katika diwani ya Saadani Kandoro, methali zimejengewa nafasi kubwa katika kujenga dhamira ambazo zinaendelea kuwa muhimu hata katika muktadha wa jamii ya kisasa.

Methali zifuatazo zimebainishwa kutoka katika diwani ya Mashairi ya Saadani.

*1. Dunia mti mkavu (uk.15)*
*2. Tenda wema wende zako usigoje shukurani (uk. 18)*
*3. Ada ya deni kulipa (uk. 27)*
*4. Haraka haraka haina Baraka (uk. 35)*
*5. Muuzaji ndiye fundi, mnunuzi siyo mjanja (uk. 61)*
*6. Haki huvunja milima (uk. 67)*
*7. Panya akitaka jina, hujipitisha kwa watu (uk. 71)*
*8. Baada ya kisa mkasa (uk. 74)*
*9. Subira yavuta heri (uk. 76)*
*10. Usiku ukikomaa, karibu kupambazuka (uk. 77)*
*11. Utu ni koja na taji (uk. 79)*
*12. Palipoingia kovu, haparudi kuwa sawa (uk. 101)*
*13. Chungu la kovu si donda (uk. 103)*
*14. Mkosaji akijuta, majuto pia ni dua (uk. 105)*
*15. Baada ya dhiki faraja (uk. 130)*
*16. Safari ni hatua (uk. 134)*
*17. Umoja ni nguvu (uk. 144)*
*18. Sheria ni msumeno (uk. 164)*
*19. Asiyesikia la mkuu huvunjika guu*

Hizi ni jumla ya methali 19 ambazo zimebainishwa kutoka katika diwani ya Mashairi ya Saadani na kupitia methali hizi tunapata dhamira mbalimbali kama zinavyofafanuliwa katika sehemu inayofuata.

**Dhamira ya Wema kama Nguzo ya Maisha ya Jamii ya Kisasa**

Binadamu ni kiumbe wa kijamii ambaye hawezi kuishi bila kushirikiana na wengine katika nyanja mbalimbali za maisha kama vile siasa, uchumi, utamaduni na dini. Uhusiano huu baina ya wanajamii hujengwa na kuimarishwa kwa misingi ya maadili na utu, ambapo kutenda wema hujitokeza kama mojawapo ya misingi hiyo muhimu. Katika Diwani ya Saadani Kandoro, dhamira ya wema imejengewa kwa kina kupitia matumizi ya methali zinazobeba mafunzo ya kijamii yenye mashiko hata katika jamii ya kisasa inayoathiriwa na mtindo wa maisha wa kidijitali na mmomonyoko wa maadili.

Katika shairi la "Binadamu Tenda Wema" (uk. 18), methali "Binadamu tenda wema, japo utendewe ubaya" hujitokeza kama kichwa cha shairi, na pia hurudiwa katika vibwagizo vya kila ubeti. Urejelevu huu wa kimethali unasisitiza kwa uzito dhamira ya wema kama silaha ya kupambana na uovu unaokumba jamii ya sasa. Kwa mfano:

*"Nitungayo si mabaya, ni mafunzo ya hekima,*
*Mtu asiye na haya, huyo si mtu ni kima,*
*Asiyejua vibaya, ni mjinga wa heshima,*
*Binadamu tenda wema, japo utendewe ubaya."*

Katika beti hizi, mshairi anaunda taswira ya kijamii inayomchukulia mtu asiye na wema kama asiye na utu, akifananishwa na mnyama. Hii ni ishara kuwa wema si tu sifa nzuri, bali ni msingi wa ubinadamu na heshima katika jamii. Kwa kuzingatia muktadha wa jamii ya leo, ambapo maadili yanazidi kupungua, methali hii huibua tafakari juu ya nafasi ya mtu mwema katika dunia yenye changamoto nyingi za kimaadili.

Katika ubeti mwingine, mshairi anasema:

*"Mkosa jema tabiya, umuepuke mapema,"*

Hii ni kauli yenye kuonesha kuwa kutenda wema huweza pia kuwa nyenzo ya kuhimiza mabadiliko ya kitabia kwa wahusika wabaya. Methali hii inaonyesha matumaini kuwa hata walio katika njia ya uovu wanaweza kubadilika kupitia mfano wa wema unaoonyeshwa na wengine. Ni picha inayowiana na dhana ya usosholojia ya fasihi, ambapo kazi ya fasihi huchukuliwa kama chombo cha kuongoza, kukosoa na kubadili mienendo ya kijamii.

Katika ubeti wa nne na saba, mshairi anasisitiza kuwa kutenda wema si jambo la maneno tu, bali ni vitendo halisi kama vile kusaidia wahitaji, kuelimisha watoto wa maskini, au hata kuwaombea dua njema waliotenda mabaya:

*4."Japo utendewe ubaya, binadamu tenda wema,*
*Kwa vitendo na hekaya, uwe mtu wa huruma,*
*Uwaombee wabaya, wapate tabia njema..."*
*7"Ukitendewa ubaya, nawe ukatenda wema,"*
*Yawe yako mazoweya, maisha dumu daima..*."

Kauli hizi hujenga picha ya jamii bora inayoweza kudumu katika mshikamano endapo wanajamii wataweka mbele utu, subira na huruma – sifa ambazo methali hii inajenga kama dhamira kuu ya mashairi. Kwa mfano, ubeti wa nne wa shairi hili kupitia methali ya "Binadamu tenda wema, japo utendewe ubaya," inaeleza kuwa kutenda wema ni vitendo na huruma ambayo mtu huwa nayo kwa watu wengine. Vitendo vinaweza kuwa vya aina mbalimbali kama vile kuwasaidia wale wasiojiweza, kuwahurumia, kuwasomesha watoto wa masikini na wale wa mitaani. Pia, kutenda wema ni pamoja na kuwaombea dua njema watenda mabaya wabadilike na kuwa na tabia njema. Hii ni daraja ya juu ya mtu mwenye kutenda wema katika jamii na kama kila mwanajamii akiwa na hulka na tabia kama hii ni dhahiri kuwa maisha yatakuwa mazuri yenye furaha na baraka tele.

Hata hivyo, mshairi anaacha nafasi ya tafakuri, akiwalazimisha wasomaji kujiuliza: Je, katika ulimwengu wa leo, bado kuna watu wenye moyo wa kutenda wema daima hata wakitendewa ubaya kila mara? Katika muktadha wa kijamii wa sasa, wanasosholojia wanasema kuwa binadamu ni kiumbe anayeathirika na mazingira yake, na mara nyingi hukata tamaa au kubadilika kwa sababu ya kuchoshwa na hali ya kutendewa mabaya. Hata hivyo, ujumbe wa mshairi unabaki kuwa wa matumaini – kuwa pamoja na ugumu wa mazingira, bado wapo watu wanaoweza kuamua kubaki waaminifu

kwa misingi ya wema. Methali hii basi, inatumika kama chombo cha ukosoaji wa jamii isiyotenda haki, na wakati huohuo, kama mwongozo wa kimaadili kwa jamii inayoishi katika muktadha wa kisasa unaokaribisha maadili mapya yasiyo na mizizi ya utu.

Katika ubeti wa saba wa shairi linalohusika mtunzi anasema:
*7. Ukitendewa ubaya, nawe ukatenda wema, Yawe yako mazoweya, maisha dumu daima, Kwa mola nakuapiya, utakuwa na heshima, Binadamu tenda wema, japo utendewe ubaya.*
Binadamu anatakiwa kutenda wema katika maisha yake ya kila siku hata kama akitendewa ubaya na watu wengine. Jambo hili limerudiwa mara nyingi katika shairi husika na kwa kutumia methali "Binadamu tenda wema, japo utendewe ubaya," kitu kinachoashiria kuwa wema ni kitu chenye nguvu kubwa ya kuubadili ulimwengu kuwa mahali pazuri pa kuishi na kila mtu akawa furahani. Hata hivyo, jambo la kuijiuliza ni kuwa hivi katika jamii ni rahisi kumpata mtu huyo? Yaani mtu ambaye anatenda wema tu hata kama anatendewa ubaya tena kila siku katika maisha yake.
Wanasosholojia wanasema kuwa binadamu ni kiumbe ambaye anachoka haraka na kukinai mambo ikiwemo hili la kutenda wema na kutendewa ubaya. Binadamu wenye tabia hii kiuhalisia hawapo katika huu ulimwengu wa leo, na kama wapo basi ni wachache sana. Yaani kama hawapo. Hata hivyo ni muhimu kuendelea kuhamasisha watu kutenda wema, kwani katika wengi wapo wachache ambao wanaweza kubadilika na kuwa na mwenendo mzuri wa kutenda wema na kuachana na mabaya.
Utu ni dhamira nyingine ambayo imenasibishwa na wema. Hali hii inadhihirika katika methali ya namba 11 uk 79 kwenye kichwa kisemacho "Utu ni koja na taji," pale mshairi anaposema:
*1. Utu ni koja na taji, koja ni kwa mtu mke, Mtu mke huhitaji, taji pia tumvike, Na mume anataraji, taji kwako tuliweke, Uaminifu tushike, utu ni koja na taji*
*4. Nawe muombe mpaji, kwa watu uaminike, Tupewe wote vipaji, ovyo tusiropoke, Tuombe kwa muombaji, mema yasituponyoke, Uaminifu tushike, utu ni koja na taji.*
Dhana ya Utu ni pana inayohusiana na maadili, heshima, na ubinadamu. Katika muktadha wa Kiafrika, utu unahusishwa na falsafa ya **Ubuntu**, ambayo inasisitiza mshikamano, huruma, na kujali wengine bila ya kujipendelea. Aidha, utu ndio msingi wa ubinaadamu unaodhirika kupitia matendo ya wema, haki, na kuheshimu wengine bila kujali tofauti zao. Kwa kweli ndio kiini cha mahusiano mazuri katika jamii, kinachoshadidia na kusimamia mshikamano wa kweli wenye kuleta utulivu na amani. Utu sio ule mshikamano wa unafiki ambao ulijengwa na ubinafsi.

Beti hizi mbili zinaendelea kutoa msisitizo juu ya umuhimu wa wanajamii kutenda wema kupitia matendo yao na si maneno pekee. Methali "Utu ni koja na taji," inaeleza kuwa utu ndio msingi wa kutenda wema ambapo binadamu hupata heshima kutokana na vitendo au matendo yake ya kiutu. Haiwezekani mtu akawa anazungumza maneno mazuri, lakini anatenda maovu akawa ni mtu mwema katika jamii. Mtu wa aina hii hupuuzwa na kuonekana kuwa hana maana na watu humdharau. Katika maisha halisi ya jamii mbalimbali duniani wapo watu ambao kazi yao kubwa ni kusema zaidi na hasa katika kuhamasisha watu kutenda mena, lakini wao binafsi wanakuwa ni watenda maovu. Haya yanadhihirika katika maandishi matakatifu pale Mwenyezi-Mungu aliposema katika Qur'an:*"Mboona mnasema msiyoyatenda?"* **(**As-Saff, 61:2**).** Aya hii inahimiza uadilifu na ukweli, ambayo ni msingi wa utu. Mtu mwenye utu hutimiza anachosema, kuepuka unafiki na kutenda kwa uaminifu. Hii inajenga jamii yenye kuheshimiana na kuaminiana. Aya hii inahimiza uadilifu na ukweli katika matendo yetu, ikitufundisha kuwa hatupaswi kusema mambo ambayo hatuna nia ya kuyatekeleza. Ni sehemu ya mafunzo ya Uislamu kuhusu umuhimu wa kuwa waaminifu na kutekeleza ahadi zetu.

Kwa upande wa Wanasosholojia wanaeleza kuwa, si jambo jepesi kwa binadamu kuendana au kutekeleza kile anachosema kwa asilimia 100 isipokuwa kwa watu wachache sana. Hii ni kwa sababu binadamu ni kiumbe ambaye anapenda kuona mambo yanakuwa vizuri. Hata hivyo suala la matamanio ya nafsi yake humfanya binadamu kutamani kufanya mambo ambayo kimsingi hayakubaliki katika jamii yake. Nafsi hiyo ya matamanio inapomzonga na kumshinda nguvu ndio hapo sasa hata ile hali ya kutenda kama alivyokuwa akisema inakuwa haipo tena. Kwa mnasaba wa maelezo haya ni kwamba bado wapo baadhi ya watu wachache ambao wanajitahidi kutenda mema kwa kadri ya uwezo wao na jamii inatambua hivyo. Kwa hiyo, dhamira ya wema kama inavyojengwa katika methali ya "Binadamu tenda wema, japo utendewe ubaya", haibaki kuwa fundisho la kimaandishi tu, bali ni wito wa mabadiliko ya kijamii unaohitaji kufanyiwa kazi kwa vitendo.

**Dhamira ya Umoja katika Muktadha wa Jamii**
Umoja na mshikamano ni miongoni mwa dhamira ambazo zimekuwa zikichukua nafasi kubwa katika kazi za fasihi simulizi na andishi katika tanzu zake za ushairi, riwaya, tamthiliya, hadithi, semi na sanaa za maonesho (Mulokozi, 1996). Umoja na mshikamano ni kitu ambacho kinatajwa kuwa ni chachu au chanzo cha maendeleo katika jamii yoyote ile iwayo duniani. Saadani Kandoro kwa kulifahamu hili ametumia methali "Umoja ni nguvu," iliyopo namba 17 katika shairi "Mambo Yanapokutana," lililopo katika ukurasa wa 144-143 kama ifuatavyo:
*1. Aha! Afia na watu, hakika yakikutana, Watu pindi awe mtu, chakula kupatikana, Furaha nyumbani mwetu, na tabia kulingana, Aha! Umoja ni nguvu, vigumu kushindikana.*
*2. Vigumu kushindikana, watu wakiwa pamoja, Maarifa hupeana, wakavizua vioja, Kazi wakifanyiana, huzifanya kwa umoja, Aha! TANU na watu, jinsi walivyokutana.*
Tukichunguza kwa undani tubaini kwamba ubeti unaasisitiza thamani ya afya na watu katika jamii, ambapo mshairi anaonyesha kuwa panapokuwa na watu wenye afya njema, maisha huwa bora na yenye mafanikio. Anaonesha kuwa mtu mmoja hawezi kuishi peke yake, bali ni kupitia jamii ndipo utu wake hutambulika – "watu pindi awe mtu." Furaha ya kweli nyumbani hailengi mali tu, bali hutegemea tabia nzuri na maelewano, ambayo hutokana na mshikamano. Hili linaungwa mkono na kauli ya mwisho ya beti hiyo: "Umoja ni nguvu". Umoja ikishamiri vigumu kushindikana", ni kiini cha dhamira – bila umoja hakuna ushindi au maendeleo.

Ama katika ubeti wa pili mshairi, anaendeleza dhana ya mshikamano kwa kuonesha kuwa watu wanapoungana, hushinda vizingiti vyote vigumu kushindikana. Pia maarifa yanaposhirikishwa, jamii husonga mbele huku akigusia umuhimu wa elimu na ushirikiano. Saadani, kwa vile amekulia katika siasa ya mfumo wa chama kimoja kwa wakati huo, anatoa mfano wa kihistoria: TANU, ambayo iliwaunganisha watu wa Tanganyika kwa malengo ya ukombozi wa kitaifa kwa sababu walikuwa na umoja wa kijamii kwa kurejlea siasa ya kijamaa. Ubeti unaonesha kuwa umoja si tu wa kaya au kijiji, bali unaweza kuathiri historia nzima ya taifa. Mashairi haya mawili yanaendeleza dhamira ya "umoja ni nguvu" kwa kutumia lugha fasaha na mifano hai kutoka maisha ya kila siku pamoja na historia ya kisiasa ya Tanzania. Ujumbe unaotolewa ni kuwa mafanikio binafsi na ya kijamii yanategemea mshikamano, ushirikiano, na moyo wa pamoja. Kama ilivyokuwa kwa TANU, hata leo, jamii yoyote inayotanguliza umoja wake ina nafasi kubwa ya kustawi.

Kimantiki beti hizi mbili zinatoa picha halisi ya methali "*Umoja ni nguvu"* kwa kuzingatia muktadha wa zama za leo tulizonazo. Zama ambazo hudhaniwa methali zimepitwa na wakati. Kwa kujengea hoja tunayosema ni kwamba, kwenye beti ya kwanza, mshairi anaonyesha kuwa mshikamano kati ya watu huleta ustawi wa jamii. Anakemea kuwa mtu hawezi kujitosheleza peke yake; bali mafanikio na furaha hutokana na kushirikiana. Katika dunia ya sasa, hii inahusiana na jinsi ushirikiano wa jamii unavyowezesha maendeleo – iwe ni kwa kushirikiana kiuchumi, kusaidiana kijamii, au kujenga uhusiano wa amani.

Katika beti ya sita Sadani anatumia taashira ya jembe na kilimo kama taswira yenyekuonyesha kuwa kazi inakuwa nyepesi pale watu wanaposhirikiana. Beti hizi mbili katika shairi hili tukizitoa katika mandhari au muktadha wa shambani na kuzinasibisha na mandhari au muktadha wa kisasa tunapata maana pevu na pana zaidi. Dhamira ya Umoja ni nguvu katika shairi hili inahusiana na zama za sasa ambapo ushirikiano katika kazi na miradi mbalimbali huleta ufanisi zaidi.

Pia, mshairi anaendelea kutumia kipengele cha semiotiki anaonyesha umuhimu wa mshikamano kwa kutumia mfano wa "wali na embe" – akisisitiza kuwa kushirikiana huleta matokeo mazuri, kama ladha nzuri ya vyakula vinapochanganywa.

Hivyo, dhamira ya "Umoja ni nguvu" bado inafanya kazi yake katika maisha ya kisasa kwa kutufundisha kuwa mshikamano ni njia ya kupata ustawi, mafanikio na maendeleo katika jamii yetu. Hapa inaoneshwa kuwa, umoja ni nguvu na wawili wanapokutana hata kama wote hawana uwezo mkubwa wa mali, lakini wanapounganisha kidogo walichokuwa nacho huwasaidia sana katika kufika malengo yao. "Huitwi mwanamkembe, jembe lolote hufana," iwe ni jembe la mkono la mpini, jembe la plau la kukokotwa na ng'ombe au jembe la trekta huweza kufanya kazi vizuri na kwa kiwango kinachotakiwa kwa sababu tu ya kushirikiana kwa pamoja. Wanakijiji hufurahia sana mavuno pindi wakati huo unapofika, lakini furaha hufana zaidi pale ambapo kila mwanajamii anapokuwa amepata mavuno. Pia, mshororo huu, "Kijijini na tuimbe, mikono tukishikana." unajenga taswira ya wanajamii kushangilia mafanikio yaliyotokana na mavuno. Kumbe kazi hufanywa kwa umoja na mshikamano, lakini pia sherehe za kusherehekea mavuno nazo pía hufanywa kwa kushiririkiana vile vile. Hii ni ishara tosha kuwa "Umoja ni nguvu," na hakuna jambo lolote ambalo linashindikana katika umoja. Wanasosholojia wanaeleza kuwa jamii inapoamua kufanya jambo lolote lile kwa umoja wao kama wanakijiji au wanakikundi mara nyingi hufanikiwa katika jambo linalohusika. Mafanikio huwa ni makubwa na kila mwanajamii hufurahia na kufarijika kwa dhati ya moyo wake. Jambo la umoja na mshikamano katika jamii ni kitu muhimu na jamii inapaswa kuendelea kushirikiana katika masuala mbalimbali kwa ajili ya maendeleo yao wao wenyewe.

Vilevile, methali umoja ni nguvu inatajwa kusaidia kuleta furaha katika familia na jamii kwa jumla. Hili linaonekana pale ambapo wanajamii wanaposhirikiana katika kufanya mambo mbalimbali kila mmoja hupata furaha ya moyoni na kuishi maisha ya raha. Hili hutokea pale ambapo kunakuwa hakuna malalamiko kuwa fulani au familia fulani wanategea kufanya kazi bali wote wanakuwa wapo kazini. Mshororo, *"Furaha nyumbani mwetu, na tabia kulingana,"* inasherehesha methali ya umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu. Umoja huwajenga watu wakawa na tabia zinazofanana kwa sababu wanakuwa wanashirikiana katika kila jambo na hivyo ni rahisi sana kuwa na muungano au mfanano wa tabia zao. Wanasosholojia wanaeleza kuwa watu wanapokuwa katika kikundi fulani na kuwa pamoja kwa muda mwingi wa maisha yao ya kila siku basi ni dhahiri watu hao watakuwa na ufanano mkubwa wa mienendo na tabia zao.

Vijana wanapaswa kuungana pamoja katika kufanya kazi na kukuza mtaji wao ili waweze kujitegemea. Hii ni kwa sababu kuungana pamoja si tu kwamba huwafanya watu kukuza mtaji wa fedha bali pia mtaji wa mawazo na maarifa. Nguvu inayosemwa katika methali "Umoja ni nguvu," ni nguvu ya kila kitu ikiwa ni pamoja na ujasiri, ushupavu, uthubutu, ubunifu na ugunduzi unaopatikana pale watu wanapoungana pamoja na kuamua kufanya jambo liwe la kiuchumi, kijamii, kisiasa au kiutamaduni. Neno "nguvu," katika methali "Umoja ni nguvu," linatupatia misimbo mbalimbali ambayo kwa hakika inatukumbusha kuwa daima umoja huleta maendeleo katika jamii ya wanadamu.

Ubeti wa pili unaendelea kusherehesha methali ya "Umoja ni nguvu," hasa katika ulimwengu wa siasa ambapo inaelezwa kuwa mtaji wa siasa ni watu. Chama cha TANU kinatajwa kufanikiwa katika kutimiza malengo na azma yake ya kuwakomboa Watanganyika kwa sababu ya kukubaliwa na watu. Methali "Umoja ni nguvu," inajimbambanua katika mshororo "Maarifa hupeana, wakavizua vioja," na hapa, nadharia ya Simiotiki kupitia msimbo wake wa kiishara unasaidia kuelewa kuwa kinachosemwa hapa ni kwamba, "nguvu," ni maarifa na ujuzi ambao hupatikana kwa kuungana pamoja. Si jambo jepesi kwa chama cha siasa kama TANU kuweza kutimiza malengo yake bila ya kuwa na watu wa kutoa mawazo na maoni ya namna bora ya kufanya mambo kwa tija na ufanisi.

Kwa kuhitimisha dhamira ya Umoja katika jamii Kandoro anaibua methali kama mbinu ya kuhimiza jamii kurudisha maadili ya mshikamano, hasa katika enzi hizi ambapo mijadala ya mitandao mara nyingi hujenga chuki badala ya mshikamano, mgawanyiko wa kisiasa, kidini na kikabila.

Vijana wa leo wanapotumia methali hii katika mijadala ya kijamii mtandaoni, wanafufua dhamira ya mshikamano kama kigezo muhimu cha ustawi wa kijamii.

**Dhamira ya Haki na Sheria katika Jamii ya kisasa**

Katika muktadha wa jamii ya kisasa, dhana ya haki na sheria imeendelea kuwa mhimili muhimu wa uhusiano wa kijamii na msingi wa ustawi wa jamii. Methali kama vipengele vya semi-fasihi, vina nafasi adhimu katika kuendeleza mijadala kuhusu maadili, usawa, na wajibu wa kila mwanajamii. Diwani ya *Saadani Kandoro* imetumia methali kwa ustadi mkubwa ili kuibua dhamira hizi muhimu, ikiendana na hali halisi ya jamii za sasa ambazo zinakabiliwa na changamoto za kisiasa, kijamii na kimaadili.

Methali: *"Haki huvunja milima"*

Methali hii ni ya sita katika orodha ya uainishaji wetu na inapatikana katika shairi **"**Haki Huvunja Milima" (uk. 67). Methali hii imetumika kama kibwagizo katika mashairi yote, jambo linalodhihirisha uzito wa dhamira ya haki inayobebwa. Katika beti:

*"Haki huvunja milima, niliambiwa shuleni"*,
*"Kwamba, haki duniani, watu wengi huwachoma..."*

Methali hii inatufundisha kuwa haki ni nguvu isiyozuilika, inayoweza kuvunja hata vikwazo vikubwa kama *milima*. Msimbo huu wa kimatukio unalinganisha ugumu wa kupata haki na kazi ya kuvunja milima—kazi ambayo huhitaji vifaa maalum na nguvu kubwa, sawa na juhudi zinazohitajika kudai haki katika jamii zisizoheshimu misingi ya usawa.

Katika muktadha wa kijamii wa sasa, methali hii inahimiza wananchi kuendelea kuwa imara katika kudai haki zao licha ya vizingiti. Ibara ya "watu wengi huwachoma" ni onyo la athari zinazoweza kuwapata wale wanaopuuza haki za wengine, ikiashiria madhila kama magereza, shutuma, au hata vifo vinavyotokana na kutotendewa haki. Wanasosholojia wanaeleza kuwa haki ni msingi wa jamii iliyojaa ustaarabu. Kwa mfano, haki ya kuishi ni ya msingi na huhitaji ulinzi kutoka kwa serikali na vyombo vya sheria. Katika jamii ya sasa, methali hii inatumika katika majukwaa ya kidijitali kuhamasisha mijadala kuhusu haki za kijamii, ikiwemo uhuru wa kuzungumza, haki za wanawake na makundi maalum.

Methali: *"Sheria ni msumeno"*

Methali hii ni ya 18 katika diwani, ikijitokeza katika utenzi wa Kandoro aliomjibu Mwalimu Julius Nyerere. Katika ubeti:

*"Ni msumeno sheria, mithali hii natia, Haitaki kubabia, pendeleo liso njia."*

Methali hii hujenga picha ya sheria kama chombo kisichopendelea, kinachokata mbele na nyuma yaani kwa wote bila ubaguzi. Dhamira inayojengwa hapa ni ya usalama wa kijamii na usawa mbele ya sheria. Katika jamii za sasa, dhana hii ina umuhimu mkubwa, hasa katika kukabiliana na changamoto za upendeleo wa kisheria, rushwa na ukandamizaji wa haki za raia.

Kwa mujibu wa wanazuoni wa sheria na sosholojia, sheria hutakiwa kuwa nyenzo ya kuweka utaratibu, siyo kifaa cha kuwakandamiza wananchi. Methali hii inatoa wito wa kuimarisha mfumo wa sheria kwa kuzingatia usawa na marekebisho ya kimfumo pale panapohitajika, sawa na msumeno unaohitaji kunolewa kila mara ili usikate ovyo.

Methali: *"Baada ya kisa mkasa"*

Methali hii ni ya nane katika orodha na inapatikana katika shairi la *"Baada ya Kisa Mkasa"* (uk. 74). Beti zake zinaonesha kuwa:

*"Baada ya kisa mkasa, ndipo tendo hufanana…"*

Methali hii huibua dhamira ya uwajibikaji na adhabu—kwamba kila tendo lina matokeo yake. Hii inasisitiza dhana ya kisasa ya uwajibikaji, ambapo kosa linapaswa kuadhibiwa ili haki ipatikane. Katika jamii nyingi, watu huathirika kwa kuhukumiwa bila ushahidi au kwa kukosa fursa ya kusikilizwa, hali inayoenda kinyume na haki za binadamu.

Hata hivyo, methali hii pia huchochea mjadala kuhusu *kisasi* na kujichukulia sheria mkononi. Katika ulimwengu wa sasa, ambapo utawala wa sheria unasisitizwa, methali hii inatafsiriwa kwa tahadhari, ikihimiza uvumilivu na kuviachia vyombo halali vya

sheria kushughulikia migogoro badala ya maamuzi ya kihisia. Tukimalizia kuhusiana na dhamira ya haki na usawa kuwa mwandishi anaonesha kuwa methali bado zina nafasi kubwa katika jamii ya kisasa kama zana ya kimaadili, kijamii na kisheria. Kwa kutumia methali kama *"Haki huvunja milima," "Sheria ni msumeno,"* na *"Baada ya kisa mkasa,"* Kandoro anazungumzia dhamira za msingi ambazo ni kitovu cha maendeleo ya kijamii. Katika muktadha wa sasa wa mijadala ya haki, usawa na utawala bora, methali hizi zimekuwa zikitumika si tu katika fasihi, bali pia katika midahalo ya kidijitali, kampeni za haki za binadamu, na harakati za kijamii. Kwa hivyo, kazi ya Kandoro inadhihirisha jinsi methali za Kiswahili zinavyoweza kubeba ujumbe wa maana kwa jamii ya sasa na kutumika kama njia ya kukuza utamaduni wa haki na utawala wa sheria.

**Dhamira ya Subira na Uvumilivu katika Muktadha wa Jamii ya Kisasa**

Dhamira ya subira na uvumilivu ni miongoni mwa dhamira kuu zinazojitokeza kwa uzito mkubwa katika *Diwani ya Saadani Kandoro*. Katika muktadha wa jamii ya kisasa, dhamira hii hujenga msingi wa maadili, msimamo na uthabiti wa kifikra na kimaamuzi miongoni mwa wanajamii. Kandoro anatumia methali mbalimbali kama *"Subira yavuta kheri", "Baada ya dhiki faraja", "Usiku ukikomaa, karibu kupambazuka", "Safari ni hatua", na "Chungu la kovu si donda",* kuibua dhamira ya subira kama jawabu la changamoto na migogoro ya kisasa. Aidha, kuhimiza maadili ya stahamala na ustahimilivu dhiki au vikwazo vya kimaisha.

1. Mifano ya Methali ya beti kama: *"Subira yavuta kheri" na "Ninaivuta subira, wakati utapinduka"*

Methali hizi zimetumika katika shairi kuangazia uvumilivu wa mhusika anapokabiliana na madhila, kashfa na hujuma kutoka kwa watu wa karibu. Hali hii inaakisi hali halisi ya jamii ya sasa ambapo wivu, fitina na kudhalilishana vinazidi kushamiri. Hata hivyo, mtunzi anasisitiza kuwa uvumilivu huleta ushindi na mabadiliko chanya. Vilevile inasisitiza kuwa kazi za fasihi hutoa miongozo ya kitabia kwa jamii. Subira katika mazingira ya kisasa ni nyenzo ya kimaadili ya kustahimili hali kama ukosefu wa ajira, migogoro ya kifamilia, au changamoto za kijamii.

2. Methali: *"Usiku ukikomaa, karibu kupambazuka"*

Methali hii imetumika katika shairi la "Usiku Ukikomaa Karibu Kupambazuka" (uk. 77), kuonyesha kuwa matatizo yanapofikia kilele, huwa ishara ya mafanikio yanayokaribia.

Beti ya kwanza inaeleza:

"*Usiku ukikomaa, karibu kupambazuka."*

Methali hii imejengwa kwa ishara ya wakati: usiku kuwa giza la matatizo, na kupambazuka kuwa nuru ya mafanikio. Katika maisha ya sasa yaliyojaa changamoto kama majanga ya kiuchumi, mabadiliko ya kijamii, au mikinzano ya kidini na kisiasa, methali hii inatoa matumaini ya kisasa kuwa hali ngumu si ya kudumu.

Kisosholojia, methali hii inaunga mkono dhana ya ustahimilivu (resilience) ambayo inasisitiza kuwa watu wenye uwezo wa kustahimili misukosuko wana nafasi kubwa ya kufanikiwa. Ushairi wa Kandoro unawaelekeza wanajamii kuwa mafanikio ni matokeo ya kusubiri, kujituma, na kutokata tamaa hata mbele ya matatizo makubwa.

3. Methali: "*Baada ya dhiki faraja*"

Methali hii ni msingi wa shairi la "Baada ya Dhiki Faraja" (uk. 129). Hapa mshairi anamrejea Muyaka, mshairi mashuhuri wa Kiswahili, kama mfano wa mtu aliyepitia dhiki lakini hatimaye akapata faraja.

Beti ya kwanza inasema:

"*Muyaka alifumbuwa, baada ya dhiki faraja."*

Methali hii inaendana na mitazamo ya kijamii kuhusu matumaini na kupona. Katika jamii ya leo, watu wengi wanakumbwa na hali za unyogovu, kufilisika, au kupoteza dira. Hivyo, methali hii inajenga imani ya kijamii kuwa hali hizo hazidumu, na faraja inaweza kupatikana endapo mtu hatakata tamaa.

Aidha, katika muktadha wa tafsiri za kijinsia, methali hii inaweza kuwa faraja kwa wanawake au vijana wanaonyimwa nafasi katika jamii, ikiwahimiza kuwa stahamala ni njia mojawapo ya kubadili hatima yao.

4. Methali: "*Chungu la Kovu si Donda*".

Methali hii imejengewa msingi katika shairi la "*Chungu la Kovu si Donda*" (uk. 102-103), ambalo linazungumzia changamoto za mahusiano ya kindoa na kifamilia. Methali hii inasisitiza uvumilivu kwa makosa ya kawaida katika mahusiano ya kibinadamu.

"Chungu la kovu si donda, kovu mtu hulishika."

Katika muktadha wa jamii ya kisasa, methali hii inaakisi changamoto nyingi za ndoa na mahusiano ya kifamilia, ambako migogoro midogo huweza kuchukuliwa kama sababu ya kutengana, badala ya kufanyiwa kazi kwa uvumilivu. Methali hii inatoa somo la msingi kuwa matatizo si lazima yawe sababu ya maamuzi magumu kama talaka, bali yanahitaji uvumilivu na mazungumzo.

Kwa mujibu wa Nadharia ya Ujenzi wa Maana ya Kijamii (social construction of meaning), methali hii inajenga maadili ya namna jamii inavyopaswa kutatua migogoro kwa uvumilivu badala ya kuvunjika kwa misingi ya kijamii kama ndoa na familia.

5. Methali: *"Safari ni Hatua"*

Methali hii ni ya 16 katika orodha ya diwani na inatumiwa kama tamathali ya semi katika kueleza kwamba mafanikio au mabadiliko huja hatua kwa hatua, si kwa ghafla. Katika maisha ya kisasa yenye kasi kubwa na matarajio ya haraka, methali hii inatufundisha kuwa kila mafanikio yana mchakato wake, na uvumilivu ni kiini cha mchakato huo.

Kwa ujumla, dhamira ya subira na uvumilivu katika *Diwani ya Saadani Kandoro* imejengwa kwa weledi wa kisanaa kwa kutumia methali zinazojikita katika mazingira ya maisha ya watu wa kawaida, lakini pia zenye uhalali mkubwa katika jamii ya kisasa. Kandoro ameweza kuzihuisha methali hizi si kama mapambo ya lugha tu, bali kama zana za kijamii (social tools) za kujenga tabia, kuhamasisha ustahimilivu, na kuhimiza matumaini katika jamii.

Kwa kutumia mtazamo wa nadharia ya kijamii ya fasihi, methali hizi zinakuwa ni njia za fasihi kushiriki katika maisha ya kijamii kwa kusawiri hali halisi ya jamii na kutoa mwelekeo wa maadili na mabadiliko. Subira na uvumilivu, kama dhamira, zinajitokeza kuwa misingi ya matumaini, mshikamano na uthabiti wa jamii ya leo kama ilivyokuwa katika jamii za jadi.

**Dhamira ya Uaminifu katika Muktadha wa Jamii ya Kisasa**

Uaminifu ni dhamira kongwe katika fasihi na hutazamwa katika namna za aina tofautitofauti. Upo uaminifu baina ya mume na mke, mazingira ya kikazi baina mwajiri na mwajiriwa, usimamizi wa amana, na pia katika kukopa na kukopeshwa. Uaminifu unatajwa kuwa ni miongoni mwa dhamira ambayo huchangia katika kuifanya jamii kuishi katika maisha ya kuaminiana, kuheshimiana na kusaidiana wakiwa wamoja tena watu wenye mshikamano na amani. Katika diwani ya Mashairi ya Saadani kuna methali ya "Dawa ya Deni ni Kulipa," ambayo ni namba 3 kwenye orodha ya ubainishaji wa methali tuliyoiandaa na inapatikana kwenye shairi "Ada ya Ahadi Deni," lililopo katika ukurasa wa 27.

Methali hii inaibua dhamira ya uaminifu kama inavyowasilishwa katika beti zifuatazo:

*1. Ahadi ni miithaki, kazi bure mwalalama, Ni deni katika haki, kulilipa ni lazima, Na kuivunja si haki, imenenwa tangu zama, Ada ya deni tazama, kulilipa ndio haki.*

*2. Kulilipa ndio haki, ahadi ina heshima, Heshima kama hutaki, vunja ahadi tazama, Tazama tazama chuki, watu watavyokuzoma, Ada ya deni tazama, kulilipa ndio haki.*

Methali imeshereheshwa vema katika beti zilizodondolewa hapo juu ikijenga dhamira ya umuhimu wa kuwa na uaminifu, hasa pale mtu anapokopeshwa fedha basi alipe deni kwani ndio uaminifu huo ambao utamfanya kuwa na heshima au kuheshimiwa katika jamii. Methali ya "Dawa ya Deni ni Kulilipa," imejengwa katika msimbo wa kiseme ikiwa na maana kuwa mtu anapodaiwa basi ni kama vile mgonjwa ambaye anahitaji dawa ili aweze kupona. Mdaiwa akishalipa deni anapona maradhi yaliyokuwa yanamsibu na hapo sasa ndio uaminifu wake unakamilika. Wanasosholojia wao wanasisitiza kuwa uaminifu ni kitu muhimu katika makubaliano yoyote ambayo jamii inayafanya na hivyo ni muhimu kila mwanajamii kutimiza ahadi yake kama ilivyowekwa au kukubaliwa katika makubaliano.

Hivyo basi kwa muktadha wa jamii ya kisasa yenye mahitaji ya maendeleo ya kiuchumi, methali hii huwahimiza watu kuwa waaminifu katika makubaliano yao ya kifedha ili kukuza ustawi wa pande zote mbili.

Methali nyingine yenye kubeba dhamira ya uaminifu ni "*Utu ni Koja na Taji"* – Shairi: Utu ni Koja na Taji lipo (uk. 79). Methali hii inapanua wigo wa uaminifu kutoka kwenye mali hadi kwenye tabia na hulka ya mtu. Katika beti kama:

*Uaminifu ni taji, mfano fedha uweke,*
*Kuropoka sitaraji, pindingu nisianguke,*
*Sipendi uteteaji, uongo nisitamke,*
*Uaminifu tushike, utu ni Koja na Taji.*

*Amana sio ulaji, ilindwe na ilindike,*
*Akija muwekewaji, mpe usimgeuke,*
*Hilo ni Koja na Taji, utu wako auvike,*
*Uaminifu tushike, utu ni Koja na Taji.*

Beti hizi zinaweka wazi kuwa uaminifu ni sehemu ya utu wa mtu. Uaminifu ni kitambulisho cha mtu mwadilifu, na ukikosekana, mtu hupoteza heshima mbele ya jamii. Methali hii inaamsha dhamira ya uaminifu katika mazingira ya utunzaji wa amana na ukweli wa kauli, ambayo ni nguzo za maisha ya kijamii ya leo yanayokabiliwa na migogoro mingi ya kimaadili.

Ama katika methali "*Muuzaji ndiye Fundi, Mnunuzi si Mjanja"* kwenye Shairi la *Soko* uk. 60–61 ni methali ambayo huibua uaminifu katika nyanja ya biashara na mahusiano ya kiuchumi. Mfano katika beti:

*Soko ni kile kiwanja, kilichopimwa kwa yadi,*
*Huwekwa vitu kwa haja, hupangwa kimaridadi,*
*Huuzwa vitu kwa tija, ili kukidhi mradi,*
*Muuzaji ndiye fundi, mnunuzi si mjanja.*

Mwandishi hapa anachosisitiza katika hi methali ni wajibu wa muuzaji kuwa mwadilifu, mkweli na mwenye kutanguliza maadili katika biashara. Mshairi anawasilisha uaminifu kama dhamira inayojitokeza kupitia usahihi wa bidhaa, uhalisia wa maelezo na bei ya haki. Katika jamii ya kisasa tunashuhudia ghushi, uchakachuaji, utapeli, udanganyifu, ukora na hata kiini macho katika biashara nyingi zinazoendeshwa mjini na hata vijijini, kwenye masoko huru na hata mtandaoni zimekithiri zinaendeshwa kwa ulaghai. Methali hii haijawachwa nyuma inatoa mafunzo ya maadili ya biashara yanayojikita kwenye uaminifu, ukweli na uadilifu.

Kwa ujumla, dhamira ya uaminifu inayowasilishwa kupitia methali hizi huendelea bado zina umuhimu mkubwa katika muktadha wa jamii ya kisasa hasa kujenga jamii ya kuaminiana na maadili yenye msingi imara wa maendeleo endelevu. Hii ni ithibati kuwa methali si tu urithi wa zamani bali ni chombo hai cha mafunzo na ujenzi wa tabia bora za kijamii hata katika karne ya sasa.

**Dhamira ya Kujipendekeza katika Muktadha wa Jamii ya Kisasa**

Kujipendekeza ni miongoni mwa tabia zinazojitokeza kwa uwazi katika jamii ya wanadamu wa nyakati zote, lakini ina sura mahsusi katika jamii ya kisasa iliyojaa ushindani wa kijamii, kisiasa, kitaaluma na kiuchumi. Katika jamii ya sasa, kujipendekeza hutazamwa kama mkakati wa kijamii unaotumiwa na watu binafsi kujitambulisha, kujipatia nafasi, au hata kupanda ngazi za kiutawala au kijamii. Muktadha huu unaakisiwa vyema katika diwani ya *Mashairi ya Saadani* kupitia matumizi ya methali za Kiswahili zinazojenga dhamira hii kwa ustadi mkubwa wa kisanaa.

Katika shairi "Panya Akitaka Jina" (uk. 71–72), methali "Panya akitaka jina, hujipitisha kwa watu" imetumika kuibua dhamira ya kujipendekeza. Tuangalie beti zifuatazo:

*1. Kuna hadithi kwa watu, wazee welzijnena,*
*Tena ni wazee wetu, wakubwa wenye majina,*
*Akili kupita zetu, wao hawakunong'ona,*
*Panya akitaka jina, hujipitisha kwa watu.*
*3. Hujipitisha kwa watu, ili wapate muona,*
*Ona mfano wa mtu, panya apate jivuna,*
*Kuwajivunia watu, vyakula akitafuna,*
*Panya akitaka jina, hujipitisha kwa watu.*

Methali hii inajenga picha ya mhusika anayeonekana hadharani, akijitokeza kwa nia ya kutambulika au kusifiwa. Katika muktadha wa sasa, hali hii inaweza kuonekana katika ofisi, siasa, mitandao ya kijamii na hata taasisi za elimu. Mtu hujipendekeza kwa viongozi au hadhira ili kuonekana kuwa ana uwezo, uaminifu, au kipaji fulani. Hili linaweza kuwa na matokeo chanya au hasi, kutegemea nia ya mhusika. Kwa mfano, mtumishi wa umma anapojitambulisha kwa juhudi na mafanikio yake ya kweli ili apandishwe cheo, hiyo ni aina ya kujipendekeza yenye kujenga. Lakini pale ambapo kujipendekeza kunachochewa na tamaa ya madaraka au utajiri wa haraka kwa njia za ujanja na udanganyifu, hapo methali hii hutumika kumkosoa mhusika huyo. Methali ya namna hii, inakuwa kama chombo cha kuonesha mwelekeo wa tabia fulani katika jamii.

Katika muktadha huo huo, methali ya **"**Dunia mti mkavu**"** iliyopo katika shairi la *"Tosheka na Upatacho. Usililie Dunia"* katika (uk. 15), huendeleza dhamira ya kupinga tamaa na ubinafsi unaochochewa na kujipendekeza. Angalia mfano wa beti:

*1. Mti mkavu dunia, nini mithali ya hicho,*
*Kiumbe kufunga nia, kutafuta apendacho,*
*Maisha kujiwania, apate akitakacho,*
*Tosheka na upatacho, usililie dunia.*

Methali hii hufundisha kuwa dunia ni ya kupita kama mti mkavu wa kuni, na kwa hivyo tamaa zisizo na mipaka, zinazotokana na kujipendekeza kwa manufaa binafsi, hazina faida ya kudumu. Hii inaendana na hali halisi ya jamii ya sasa ambayo mara nyingi hukumbwa na kashfa za watu waliotumia njia za kujipendekeza kwa nia ya kupata cheo au nafasi au mali kwa ajili ya kujinifaisha binafsi, lakini hatimaye wakashindwa kuhimili dhamana za nafasi hizo.

Kwa mujibu wa mitazamo ya kisosholojia, jamii ya sasa inaathiriwa sana na matabaka, mitandao ya ushawishi, na mihemuko ya kihisia inayofanywa kupitia majukwaa ya kidijitali. Kujipendekeza kumevuka mipaka ya jadi na sasa kunaweza kufanyika kupitia mitandao ya kijamii, vyombo vya habari, au kupitia kampeni za kipekee za kujijengea taswira mbele ya umma.

Hivyo basi, Saadani Kandoro anafanikisha kupitia methali hizi, kujenga dhamira ya kujipendekeza kwa kuionesha kuwa ina sura mbili: chanya na hasi. Katika jamii ya sasa, methali hizi hutoa mwanga na busara ya kutambua thamani ya kujithamini kwa misingi ya uwezo wa kweli na sio kwa njia za ulaghai au unafiki. Tuna itimisha kwa kusema Saadani Kandoro anaonesha jinsi methali za Kiswahili zinavyoweza kuwa chombo cha kupima na kueleza mienendo ya binadamu katika jamii ya sasa. Hivyo ni nyenzo muhimu katika kuielimisha jamii ya kisasa kuhusu mipaka ya kujipendekeza na maana halisi ya kujithamini kwa msingi wa utu na uadilifu.

**Dhamira ya Hekima na Busara katika Muktadha wa Jamii ya Kisasa**

Dhamira ya hekima na busara ni msingi muhimu unaojitokeza katika methali nyingi za Kiswahili. Hata ile maana ya methali ni nini basi ianatambuliwa kuwa ni semi za hekima na busara.... Methali imepewa uzito mkubwa katika fasihi ya Kiswahili tangu enzi za wahenga hadi wakati wa sasa. Hekima na busara huelekezwa kama msingi wa maadili, maamuzi sahihi, na utatuzi wa changamoto mbalimbali zinazojitokeza katika jamii. Hata katika mafundisho ya Uisilamu suala la hekima limepewa uzito sana. MwenyeziMungu aliposema kwenye Qur'an *" Yeye Humruzuku hekima amtakaye; na mwenye kupewa hekima, basi bila shaka amepewa kheri nyingi sana."*

(*Al-Baqarah 2:269*). Hekima katika aya hii ina maana pana, ikiwa ni pamoja na: uamuzi sahihi, ufahamu wa mambo, tabia njema, uadilifu na maarifa yaelekezaoa njia ya kumpendeza Mola. Umuhimu wa kutumia hekima unaonekana katika aya nyingine ya Qur'an, Mwenyezi Mungu anatoa mwongozo wa kulingania watu kwa kusema:

*"Lingania katika njia ya Mola wako kwa hekima na mawaidha mazuri..."* (An-Nahl 16:125). Hivyo hekima yatakiwa kwa kila

mzungumzaji na mliganiaji wakati wa kuzungumza au kulingania watu. Ni jambo bora kwa mzungumzaji au mlinganiaje ajipambe na sifa hiyo. Kinyume chake inapokosekena hekima mambo huenda ovyoovyo na huenda kusababisha vurugu au kutoelewana.

Mwenyezi Mungu anafafanua kuwa hekima ni neema kubwa, na kupewa hekima ni kupata kheri nyingi kuliko mali, cheo au utajiri wa dunia. Katika muktadha wa jamii ya kisasa ambayo imejawa na papara, ushindani, na shinikizo la mafanikio ya haraka, methali hizi hutoa mafunzo ya kina kuhusu umuhimu wa kutafakari kabla ya kutenda.

Methali ya *"Haraka haraka haina baraka"* kama inavyojitokeza katika shairi la "Mwendo" (uk. 35) iliyopo katika mshororo wa kwanza wa ubeti wa kwanza ni mfano mahsusi wa ujenzi wa dhamira ya hekima na busara katika Mashairi Kandoro.

1. *Mwendo mwema si haraka, njiani unapokwenda,*
*Unaweza kutapika, au kupata kidonda,*
*Na mbele hautofika, ukaishia kudoda,*
*Kiumbe kinachokwenda, hutazamiwa kufika.*

Katika ubeti huu, methali hii inatumika kuonesha kuwa maamuzi ya haraka bila busara huzaa madhara. Madhara haya yakiwemo hasara, majuto au kushindwa kufanikisha malengo. Jambo hii linaakisi hali ya jamii ya sasa ambayo watu wengi hujikuta wakifanya maamuzi ya haraka kutokana na mashinikizo ya kijamii au tamaa ya mafanikio ya muda mfupi, bila kutafakari madhara ya muda mrefu.

Neno "mwendo" katika shairi hili limetumika kwa namna ya tashbihi na ishara, kuwakilisha safari ya maisha, hatua za maendeleo, au mchakato wa kufanikisha jambo fulani. Mwanadamu anapoongozwa na hekima na busara, huweza kupiga hatua zenye tija, kwa utulivu na tahadhari. Methali hii huambatana pia na methali nyingine kama vile "Pole pole ndiyo mwendo", inayosisitiza kwa njia nyingine tena kuwa uvumilivu na kutafakari ni nguzo za mafanikio ya kweli.

Kwa mujibu wa ubeti wa tatu:
*Unapotaka kufika, nenda kama ukiwinda,*
*Na uijue mipaka, ya njia unayokwenda,*
*Ili usije kuruka, na ukafungwa mikanda,*
*Kiumbe kinachokwenda, hutazamiwa kufika.*

Mstari huu unaendeleza wazo la msingi kwamba hekima huhitaji utulivu, uangalifu na uelewa wa mipaka. Hii ni hoja muhimu katika jamii ya leo ambako watu wengi hupoteza dira kwa kukosa uvumilivu au kufanya mambo kwa pupa. Kwa kutumia methali hii, mwandishi anaibua na kuendeleza dhamira ya hekima na busara kwa namna inayoamsha tafakari miongoni mwa wanajamii wa kizazi cha sasa. Zaidi ya hayo, dhamira hii ni muhimu katika jamii ya sasa inayokumbwa na migogoro ya maadili, mporomoko wa nidhamu, na ukosefu wa subira katika mambo ya maendeleo. Methali hii huibua hitaji la watu kutafakari, kujenga hulka ya usikivu, na kuthamini ushauri wa wengine kabla ya kuchukua hatua kubwa katika maisha au kazi.

Kwa kuhitimisha dhamira ya hekima na busara tunajifunza kwamba, methali kama "Haraka haraka haina baraka" na matumizi yake katika diwani ya *Mashairi ya Saadani Kandoro* si tu zinatufundisha maana ya busara, bali pia zinaakisi changamoto na hali halisi ya maisha ya kisasa. Hekima na busara kama dhamira kuu ya methali hizi hujenga msingi wa utulivu wa kijamii, ufanisi wa kiuchumi, na maelewano ya kifamilia na kitaasisi. Ujenzi wa dham ira hii katika kazi ya Kandoro unatoa mchango wa pekee katika kuendeleza maadili ya Kiswahili kwa njia inayowiana na mahitaji ya dunia ya sasa.

**Mjadala wa Matokeo ya Utafiti**

Matokeo ya utafiti huu yanaonesha kuwa methali katika *Diwani ya Saadani Kandoro* hazikubaki katika nafasi ya mapambo ya lugha pekee, bali ni nyenzo madhubuti za ujenzi wa dhamira zinazolenga kutoa mafunzo, kukemea tabia potovu katika jamii, na kutafakari hali halisi ya jamii ya kisasa. Methali zimejengewa nafasi mahsusi ya kuibua mjadala kuhusu masuala ya kijamii, kisiasa, kimaadili, kiutamaduni, na hivyo kutimiza jukumu la fasihi kama kioo cha jamii ya kisasa.

Kwa mfano, methali kama *"Mti wenye matunda hupigwa mawe"* linaebua dhamira kama vile wivu wa kijamii dhidi ya unyanyasaji wa mafanikio jambo ambalo linalofungua mjadala mpana kuhusu usawa, haki na heshima ya mafanikio katika jamii ya leo. Methali hii hujenga dhamira ya kushughulikia mizizi ya chuki za kitabaka na ukosefu wa utu miongoni mwa watu wanaoendelea. Hili linathibitisha kuwa ushairi wa Kiswahili wa maandishi unaweza kuhuisha methali kama urithi wa fasihi simulizi kwa kuzitumia kwa namna ya kuhamasisha mabadiliko ya kijamii.

Vilevile, methali kama *"Samaki mkunje angali mbichi"* hujenga dhamira ya malezi ya maadili katika utotoni, ikiashiria wajibu wa jamii katika kufundisha maadili mapema kabla ya tabia mbaya kuota mizizi. Methali hii inaipa methali nafasi ya kushughulikia pengo lililopo kati ya maarifa ya jadi ya maadili na mfumo wa elimu rasmi unaotawaliwa na maadili ya kimagharibi, hivyo kuibua changamoto kuhusu nafasi ya urithi wa jadi katika elimu ya sasa. Hivyo basi matokeo haya yanaibua hoja muhimu kuhusu mvutano kati ya elimu ya jadi na mfumo wa elimu rasmi unaoegemea katika maadili ya kimagharibi. Methali zinapowasilisha mafunzo ya kimaadili kama vile umuhimu wa malezi bora, heshima, na uadilifu, huibua hoja kuhusu nafasi ya maarifa asilia katika mchakato wa kuunda mitaala ya elimu inayotegemea muktadha wa jamii za Kiafrika. Hali hii inathibitisha hoja za watafiti kama Mulokozi (1999) kuhusu umuhimu wa maarifa ya jadi katika kukuza utu na utambulisho wa Mwafrika.

Zaidi ya hayo, utafiti huu umeonesha kuwa methali zinaweza kutumika kwa mafanikio katika fasihi andishi ya kisasa, hasa kwa njia ya mashairi kama yanavyojitokeza katika diwani ya Kandoro. Hii ni tofauti na tafiti zilizopita kama vile za Mulokozi (1999) na Khamis (2005) ambazo zilitilia mkazo nafasi ya methali katika simulizi za jadi na mazungumzo ya kila siku, lakini hazikuchambua kwa undani matumizi ya methali katika ushairi wa maandishi wa kisasa.Tofauti na tafiti zilizotangulia ambazo zilizingatia sana methali katika muktadha wa simulizi za jadi, utafiti huu umeonesha kuwa methali zinaweza kutumika kwa ufanisi katika ushairi wa maandishi wa kisasa, ambapo dhamira zake hubeba ujumbe unaogusa maisha ya sasa. Hii ni hatua muhimu ya kielimu inayopanua upeo wa matumizi ya methali katika fasihi andishi, hususan kwa kizazi cha leo kinacholelewa katika mfumo wa elimu rasmi na mitazamo ya kisasa.

Zaidi ya hayo, matumizi ya methali kuwasilisha ujumbe wa kisiasa na kijamii yanadhihirisha kwamba methali zinaweza kuwa njia ya ukosoaji wa kijamii, hususan katika mazingira yenye ukosefu wa haki, matumizi mabaya ya madaraka, na kuharibika kwa maadili. Kwa hivyo, methali zinabaki kuwa sauti mbadala ya jamii, zinazoelezea yale yasiyosemwa moja kwa moja, lakini yenye mashiko makubwa katika fikra na maadili ya watu.

Pamoja na hayo utafiti huu pia umebaini kuwa methali katika diwani hii huakisi muktadha wa kihistoria na kijamii, ambapo jamii ya Kiswahili ilikumbwa na changamoto za unyonyaji wa kitabaka, uongozi usio na maadili, na unafiki wa kijamii. Methali zinazochambua hila, tamaa na ulafi hujenga dhamira ya kukosoa viongozi au watu wenye mamlaka wanaokosa uadilifu, na hivyo kutoa fursa ya tafakari kuhusu mwelekeo wa maadili ya uongozi katika jamii ya sasa. Tumebaini kwamba, ujenzi wa dhamira hizi unaonesha kuwa methali bado ni hai, si tu kwa maumbo, bali pia kwa kazi yake ya kijamii na kimtazamo.

Kwa mantiki hiyo, methali zinapaswa kuendelezwa kama nyenzo ya maarifa, zifundishwe katika mfumo rasmi wa elimu, na zitumike kama zana ya kufundisha maadili na kuhamasisha mabadiliko chanya katika jamii ya sasa. Ushairi kama ule wa Saadani Kandoro unathibitisha kuwa methali zina nafasi kubwa katika kukuza fikra za kijamii na kuhimiza mabadiliko katika jamii ya Kiswahili ya leo.

**Hitimisho**

Utafiti huu umebainisha kwa kina kuwa methali ni nguzo muhimu ya ujenzi wa dhamira katika fasihi ya Kiswahili, hususan ndani ya *diwani ya Saadani Kandoro*. Katika utafiti huu methali zimebainika ni sehemu hai, endelevu, na yenye mchango mkubwa katika jamii, hasa katika mazingira ya kisasa yanayobadilika kwa kasi. Kupitia *Diwani ya Saadani Kandoro*, methali si tu maneno ya busara kutoka kwa wahenga, au mapambo ya lugha, bali kama zana hai zenye ubunifu wa mawasiliano zinazobeba ujumbe wa maadili, hekima, mshikamano wa kijamii, utu, haki, usawa wa kijinsia na tahadhari kuhusu hali halisi ya maisha ya jamii ya leo.

Dhamira kama malezi ya kijamii, usawa wa kijinsia, ukosoaji wa uongozi, umuhimu wa mshikamano na haki, pamoja na ulinzi wa utu wa binadamu zimewasilishwa kwa ustadi kupitia methali ambazo zinaendelea kuvutia fikra na kuamsha tafakuri hata kwa wasomaji wa kizazi kipya. Methali kama *"Haki haipotei"*, *"Umoja ni nguvu"*, na *"Haraka haraka haina baraka"*, zimeonyesha kuwa bado zina nafasi ya kuelimisha, kuonya, na kuongoza jamii.

Katika muktadha wa jamii ya kisasa inayokumbwa na changamoto za kiutandawazi, maendeleo ya teknolojia, na mabadiliko ya mitazamo ya kijamii, methali hizi zimepewa uhai mpya kupitia matumizi ya fasihi andishi ya kisasa, mitandao ya kijamii, na hata njia za mawasiliano ya kidijitali kama memes na vlogu. Kwa njia hiyo, methali zimekuwa chombo chenye nguvu ya kuendeleza mijadala ya kijamii, kufundisha maadili, na kuchochea mabadiliko chanya.

Hivyo basi, methali hazipaswi kuachwa kama masalio ya historia, bali zinastahili kuendelezwa na kutumiwa kwa ubunifu zaidi katika sekta za elimu, utamaduni, fasihi, na vyombo vya habari. Ni jukumu la waandishi wa fasihi, walimu, watafiti, na wanajamii kwa jumla kuzihuisha methali hizi kama hazina ya maarifa na chombo cha kujenga jamii yenye mshikamano, fikra chanya, na maendeleo ya kudumu.

Kwa ujumla, ujenzi wa dhamira za methali katika diwani ya *Saadani Kandoro* umethibitisha kwamba methali bado ni zana hai ya mawasiliano, kioo cha jamii, na dira ya kiutamaduni. Zinapaswa kuendelezwa kama urithi hai unaoweza kutumiwa kuhimiza mwelekeo sahihi wa kijamii katika enzi hizi za kisasa.

**Mapendekezo ya Utafiti**

Kwa kuzingatia matokeo ya utafiti huu na muktadha wa kijamii wa leo, yafuatayo mapendekezo:

**1. Uendelezaji wa Methali kama Nyenzo ya Kuelimisha**

Wadau wa elimu na utamaduni wanashauriwa kuzitumia methali kama nyenzo ya kufundisha maadili na utambulisho wa Kiafrika, kwa kuwa zinaakisi hekima na uhalisia wa jamii. Zingatie matumizi ya methali si tu katika fasihi simulizi, bali pia katika maandiko ya kisasa, hasa mashairi.

**2. Kuingizwa kwa Methali katika Mitaala Rasmi ya Elimu**

Mamlaka za elimu kama vile KICD (Kenya) au TIE (Tanzania) zinapaswa kujumuisha vipengele vya methali katika masomo ya lugha na fasihi, kwa lengo la kuimarisha uwezo wa wanafunzi kuelewa dhamira na mafunzo ya kijamii kupitia kazi za kisanaa kama mashairi na insha.

**3. Utafiti Zaidi Kuhusu Methali katika Fasihi Andishi ya Kisasa**

Watafiti wa Kiswahili wahimizwe kuchunguza kwa kina matumizi ya methali katika kazi mbalimbali za fasihi andishi za kisasa kama riwaya, tamthilia, na mashairi, ili kufichua mchango wake katika kuunda fikra na kuendeleza mabadiliko ya kijamii.

**4. Uendelezaji wa matumizi ya methali katika elimu ya sasa**

Mashirika ya elimu na walimu wa lugha ya Kiswahili wanapaswa kuendeleza matumizi ya methali katika mtaala wa elimu, hasa katika somo la Kiswahili, ili kuwasaidia vijana kuelewa na kuthamini hekima ya methali katika muktadha wa maisha ya sasa.

**5.Utafiti zaidi kuhusu matumizi ya methali katika majukwaa ya kisasa/Mitandao ya Kijamii**

Zinahitajika tafiti zaidi zinazochunguza namna methali zinavyotumika katika mitandao ya kijamii na majukwaa ya kidijitali kama mbinu mpya ya mawasiliano ya kijamii.

**6. Kukuza utamaduni wa matumizi ya methali katika jamii ya sasa**

Vyombo vya habari na taasisi za kijamii vina nafasi kubwa ya kusaidia kukuza matumizi ya methali kama sehemu ya mawasiliano ya kila siku, ili kuendeleza maadili na mshikamano wa kijamii katika mazingira ya kijamii yanayobadilika kwa kasi.

**Marajeo**


Adam, O. A. (2014). “Kuchunguza Dhamira za Kijamii na Kitamaduni katika Riwaya ya Kiswahili; Mifano kutoka Kuli na Vuta Nkuvute.” Tasnifu ya Uzamivu ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. Haijachapishwa.

Hassan, A. M. (2016). “Kuchunguza Falsafa ya Mapenzi katika Diwani ya Mapenzi Bora.” Tasinifu ya Uzamivu ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Kandoro, S.A. (1972). *Diwani ya Saadan*, Dar es Salaam: NPL.

Mulokozi, M. M. (1996). Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili. Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Maitaria, J. N. (2012). “Uainishaji wa Ushairi wa Kiswahili: Dhima ya Methali,” Tasinifu ya Uzamifu, Chuo Kikuu Cha Kenyatta.

Maitaria, J. N. (2010). “Methali Kama Fomula ya Uwasilishaji wa Ushairi wa Kiswahili: Mfano wa Baadhi ya Mashairi ya Abdilatif Abdalla,” katika *Kioo cha Lugha* Juzuu la Nane, Dar es Salaam: TUKI. Kur. 107-117.

Mazrui, A. A. (2020). The Pragmatics of Proverbs In Swahili Political Discourse. *Swahili Forum*, *27*, 1–15. https://www.qucosa.de/startseite/

Njogu, K., na Chmerah, C. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi, Nadharia na Mbinu. Nairobi*: JKF.

Said, A. A., & Mwenda, M. N. (2019). “The Relevance f Swahili Proverbs in Contemporary Social Communication”. *International Journal of African Language Studies*, *5*(2), 45–60.

Sengo, T. S. Y. M. (2012). Hisi Zetu, Dar es Salaam: TATAKI.

TUKI (Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili). (2013). *Kamusi ya Methali*. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Qur'an Tukufu. (n.d.). (Ghassan Al-Mutaghlib, Trans.). Al-Mutaghlib Islamic Center. (Original work published n.d.)

Qur'an Tukufu. (n.d.). (Abdullah Farsi, Trans.). Farsi Islamic Publications. (Original work published n.d.)

Wamitila, K. W. (2021). *Fasihi ya Kiswahili: Nadharia na uhakiki*. Phoenix Publishers.